# MSAMAHA WA KODI YA FORODHA KWA WATUMISHI WA UMMA

*Imewasiliswa na: Lusajo Nelson Mwasaga*
*Afisa Forodha Mwandamizi – Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa*

# MPANGILIO WA MADA

- Utangulizi-Mtumishi wa Umma
- Msingi wa Kisheria
- Kodi zinazosamehewa
- Sifa ya Gari
- Utaratibu wa kuomba msamaha
- Masharti ya Msamaha
- Sababu za Kuchelewa na Mambo ya kuzingati
- Mchanganuo wa Kodi

# UTANGULIZI

## 1. Msamaha wa Kodi (Tax Exemption)

- Ni punguzo(unafuu) au kuondolewa kabisa kwa wajibu wa kisheria wa kulipa kodi au tozo mbalimbali kwa Serikali
  - Unafuu (Punguzo): Kupewa msamaha kwa kiwango fulani; ama asilimia ya kiwango kinachotozwa au aina ya kodi inayotozwa
  - Msamaha wa Jumla: Kusamehewa kodi zote

# UTANGULIZI

- Huu ni msamaha wa kodi unaotolewa kwa waheshimiwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watumishi wa umma.

- Msamaha huu unatolewa kwa gari moja kwa kipindi cha miaka minne.

# UTANGULIZI

## 2. Mtumishi wa Umma

Ni mtu anayehudumu katika ajari ya kudumu katika taasisi zifuatavyo;

- Serikali Kuu
- Serikali za mitaa
- shirikia la serikali (ambalo bajeti yake inagaramiwa na Serikari kwa 50%-Mfano Tanesco
- Taasisi za Serikali. Mfano NECTA

NB:Watumishi wenye ngazi ya mshahara kuanzia TGS D na wawe na muda usiopungua miaka 4 kabla ya kustaafu

# NGUVU NA MSINGI WA KISHERIA

- Msamaha huu wa kodi unaongozwa na chapisho la Gazeti la Serikali (GN)

- Ushuru wa Forodha (Customs Import Duty)

  Tangazo la Serikali Na. 520 (GN. 520)

- Ushuru wa Bidhaa (Customs Excise Duty)

  Tangazo la Serikali Na. 522(GN. 522)

# KODI ZINAZO SAMEHEWA

- Ushuru wa Forodha (Customs Import Duty)
- Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty), isipokuwa ushuru wa uchakavu (excise duty on motorvehicle age)

N.B: Pamoja na kwamba tunaita ni msamaha, maana halisi siyo msamaha bali ni msaada wa kulipiwa na Serikali. Hili hufanyika kwa njia ya VOCHA YA HAZINA (Treasury Voucher Sytem) ambapo Serikali huwa na fungu la fedha maalumu kwa kazi hii.

# SIFA YA GARI ZINAZOSAMEHEWA

- 1. Saloon car
- 2. Station wagon
- 3. Pick up ambazo zinabeba mzigo chini ya tani 2
- 4. Gari ambazo uwezo wa kubeba abiria hauzidi siti 9
- 5. Gari isizidi umri wa miaka 10 tangu kutengenezwa
- 6. Gari lenye umri wa miaka 0 hadi 7 litapata msamaha bila kodi ya uchakavu
- 7. Gari ambazo ujazoe wake wa Engine hauzidi 3000cc (waheshimiwa wabunge (cc) hainaa ukomo

# Utaratibu wa kuomba Msamaha

- Baada ya kuagiza gari na kupokea nyaraka za manunuzi mnufaika wa msamaha atafanya yafuatayo;
  - Kujaza fomu za maombi ya msamaha nakala (4) zinazopatikana katika tovuti ya Mamlaka ya Mapato
  - Nyaraka za ununuzi wa gari, nyaraka za kiforodha na nyaraka muhimu za kiutumishi ili kuthibitisha utumishi wake.
  - Kuandika barua ya maombi ya msamaha kwenda kwa Afisa Masuuli wake.

# Fomu ya  Maombi ya msamaha

- Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya msamaha (Copy nne)

A. Sehemu A itajazwa na muombaji
B. Sehemu B ya fomu itajazwa Mwajiri

# UTARATIBU WA KUOMBA MSAMAHA

- Msamaha tajwa utaombwa kwa kuandaa nyaraka zifuatazo;
  - Mwombaji lazima awe na TIN
  - Picha nne za passport size zinazotokana na negative moja
  - Barua ya Utambulisho kutoka kwa muajiri (mtendaji mkuu taasisi anayofanyia kazi muombaji)
  - Slary slip ya karibuni
  - Appointment letter na barua ya kupandishwa daraja ya karinuni
  - Copy ya kitambulisho cha kazi

# UTARATIBU WA KUOMBA MSAMAHA

Nyaraka….

- Ankara ya gari (Invoice)
- Muswada wa shehena (Bill of Lading) au Muswada wa Shehena wa Ndege (Air Waybill) au Muswada wa Shehena inayoingia kwa njia ya barabara (Road Consignment Note)
- Cheti cha kusafirisha gari nje ya nchi toka nchi inakotoka na tafsiri yake kama gari inatoka Japan au UAE
- Kadi au cheti cha kufuta usajili toka nchi inakotoka
- kadi ya usajili toka nchi inakotoka.

# Utaratibu wa kuomba Msamaha

- Mtumishi anawajibika kurejesha fomu zilizojazwa Mamlaka ya Mapato Tanzania – Idara ya Kodi za Forodha kwa ajili ya kukadiriwa kodi
- TRA watawasilisha hati ya madai Wizara ya Fedha inayoonesha kiasi kinachopaswa kulipwa na Serikali kama msamaha wa kodi kwa ajili ya mtumishi
- Aidha mtumishi atapaswa kulipia kiwango kinachompasa ambacho ni jumla ya kodi zote toa kiasi cha msamaha

# MASHARTI YA MSAMAHA

- Msamaha hauhamishwi
- Msamaha utakoma ikiwa mtumishi ataacha kuwa mtumishi ndani ya miaka 4 toka kutolewa kwake.
- Msamaha huu hautolewi kwa watumishi walio masomoni au anae fanya kazi ya muda nje ya nchi.
- Kabla ya kuuza, kuhamisha umiliki au kugawa gari iliyonufaika na msamaha huu ni sharti idhini iombwe kwa Kamishna wa Forodha
- Ni muhimu kutunza kumbukumbu za misamaha kwa sababu nyingi ikiwemo ukaguzi na kuandaa taarifa za matumizi.

# SABABU ZA MAOMBI YA MISAMAHA KUCHELEWA

- Maombi kutoelekezwa ofisi sahihi
- Maombi kukosa viambatishi hitajika, kwa mujibu wa sheria
- Maelezo ya maombi kutototolewa kwa ufasaha

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA ILI KUEPUKA USUMBUFU WAKATI WA KUOMBA MSAMAHA

1. Kuandaa nyaraka zote hitajika kwa wakati

2. Kuwasilisha maombi ya msamaha kwa Kamishna wa Forodha kabla ya kuingiza mzigo (importation). Ni muhimu kuzingatia kwamba maombi ya msamaha kwenye dirisha hili hushughulikiwa katika ofisi ya Kamishna wa Forodha

3. Kuambatisha vielelezo vyote hitajika kwa mujibu wa sheria na viwe vinasomeka

4. Kufanya ufuatiliaji wa karibu

# Mchanganuo wa kodi

| | Tax Base | Rate | Amount |
|---|---|---|---|
| Umri wa gari 8 yrs | Sh. | | Sh. |
| Thamani ya gari hadi Tanzania | | | 10,000,000.00 |
| Import Duty (Kodi ya forodha) | 10,000,000 | 0.25 | 2,500,000.00 |
| Excise Duty (Kodi ya bidhaa) | 12,500,000 | 0.05 | 625,000.00 |
| Railway levy | 10,000,000 | 0.015 | 150,000.00 |
| Customs processing fee (CPF) | 8,000,000 | 0.006 | 48,000.00 |
| VAT | 13,323,000 | 0.18 | 2,398,140.00 |
| VEH (Kodi ya Usajili wa gari) | | | 500,000.00 |
| **Kiwango cha Msamaha** | | | **3,125,000.00** |
| **Kiwango atakacholipa mtumishi** | | | **3,096,140.01** |

# Asanteni

# Kwa Kunisikiliza

